FAIR COMPETITION COMMISSION

**HOTUBA YA MKAGUZI MKUU WA SHERIA YA ALAMA ZA BIDHAA, DK. FREDERICK RINGO (WAKILI) AKIKABIDHI VIFAA VYA MUZIKI KWA JESHI LA MAGEREZA, UKONGA, DAR ES SALAAM, JANUARI 29, 2016**

**Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, John Minja**
**Viongozi Mbalimbali wa Jeshi la Magereza Mliopo hapa**
**Askari wa Jeshi la Magereza**
**Waandishi wa Habari**
**Wageni Waalikwa**
**Mabibi na Mabwana**
**Itifaki Imezingatiwa**

Awali ya yote, kwa niaba ya Tume ua Ushindani napenda kupongeza kazi nzuri inayofanywa na jeshi lako katika kujenga jamii inayozingatia misingi ya sheria za nchi. Aidha, napenda kutambua kupongeza juhudi zinazofanywa na jeshi la Magereza na majeshi mengine nchini katika kukuza vipaji na weledi katika maeneo ya sanaa za maonesho na muziki, kazi za mikono, kazi za ufundi kama vile useremala, pamoja na shughuli nyingine za kiuchumi.

Kutokana na kutambua umuhimu wa shughuli zinazofanywa na majeshi hapa nchini, Tume imeona ni jambo la busara ikawaunga mkono kwa kuwapatia vifaa vya muziki vilivyo mbele yenu.

Vifaa tunavyowakabidhi leo ni pamoja na magitaa mawili, seti moja ya ngoma za muziki, spika saba pamoja na mashine moja ya kuchanganyia muziki (mini mixer).

Kama Mkaguzi Mkuu wa Sheria ya Alama za Bidhaa (ambaye pia ni Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ushindani), Wakili Dk. Frederick Ringo, leo, Ijumaa, Januari 29, 2016 amekabidhi vifaa vya muziki vyenye thamani ya Sh. Milioni 7 kwa Jeshi la Magereza.

Vifaa hiyo vilikamatwa na wakaguzi wa Tume katika operesheni iliyofanyika jijini Dar es Salam tarehe 19 Oktoba, 2010 kwa kushirikiana na wasimamizi wa Nembo za vifaa vya Peevay, Yahama na JBL, kampuni ya Credible Sounds ya Nairobi, Kenya na kuthibitishwa kukiuka Sheria ya Alama za Bidhaa, inayokataza kuingiza na kuuza nchini bidhaa zinazokiuka taratibu za umiliki na matumizi ya “miliki-bunifu” za nembo na alama za kibiashara.

Kwa mamlaka niliyopewa na Sheria ya Alama za Bidhaa ya mwaka 1963, iliyorekebishwa, na kanuni Namba 55(3) za mwaka 2008 za Sheria hiyo, nikiwa ni Mkaguzi Mkuu chini ya Sheria husika, nimechagua kuzitoa zawadi bidhaa zilizokamatwa kwa kukiuka sheria ya alama za bidhaa kwa Jeshi la Magereza, ambayo ni taasisi ya umma, badala ya kuziteketeza.

Msingi wa kifungu hiki kinachowezesha aina fulani ya bidhaa kutolewa zawadi ni kuwa si kila bidhaa inayokiuka sheria ya alama za bidhaa ni hatarishi, bali kinachofanya liwe kosa ni wizi au matumizi yasiyoidhinishwa ya alama za kibiashara zilizosajiliwa na mamlaka halali bila ridhaa ya mwenye alama/nembo. Bidhaa za aina fulani zikiwemo vifaa vya muziki vinapokamatwa vinaweza kugawiwa kama zawadi bila kuwa hatarishi. Hivyo, bidhaa zinazogawiwa hapa leo ni bidhaa zilizo salama kwa matumizi lakini hazikuruhusiwa kuingia sokoni kwa kuwa ziligushi nembo za watengenezaji halisi wa bidhaa husika na hivyo zililenga kuwadanganya wateja.

Hili ni zoezi la pili la kukabidhi vifaa vya muziki kwa vitengo vinavyojihusisha na sanaa katika majeshi yetu, ambapo tarehe 23 Juni, 2014, nilikabidhi vifaa vingine vya muziki kwa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT Oljoro), mkoani Arusha.

Nawapongeza sana kwa kupokea vifaa hivi na nina matumaini kuwa vitaendelea kukuza vipaji vya wanamuziki katika Jeshi la Magereza.

Hongereni sana, Asanteni sana. Hapa Kazi Tu!